LIDEMO.NET
LÍNGUAS DE MOÇAMBIQUE

*Kweleza Kusiyana kulipo nkati ya*

# Bibiliya na Kolowani

Ficha Técnica

Título: Kweleza Kusiyana kulipo nkati ya Bibiliya na Kolowani
(As Diferenças Entre a Biblia e o Korão)
(Differences Between the Bible and the Koran)

Língua: Kimwani

Primeira edição electrónica, 2010

Produzido por: JU WA
lidemo.net@gmail.com
C.P. 652
Nampula, Nampula
Moçambique

O utilizador pode copiar e distribuir a obra.

iwapo namuna ya kufunda vinu vya kuliga-liga-vyo. Ziwankuwoneka sana-sana kuwa Bibiliya ya lelo iwa sawa-sawa na usemi Mwenyezimungu wawapele wanadamu wenye kwandika. Ainapinduliwa wala kongeziwa kinu!

Nkati ya vitabu vya dini piya, acipo cengine cili na habali maajuza kamba Bibiliya.
Eco ndi cijuzi citiwe “Usemi wa Mwenyezimungu.”
Ewo tu basi kweli-kwelini ndi ulawilila ka Mwenyezimungu.

**4. Utikinifu ukiwepo wakati wa vyandikiwe vitabu vya Bibiliya**
Wanu wengine wanawo tafauti ya kweleliwa na usemi wa Bibiliya konta awejiwa hali za Bibiliya. Kwa nfano, Mwenyezimungu katumiza kuwapoteza wanu wa Kanã. (Walawi 20:10-17) Sababuni? Konta wanu wa Kanã watenda vinu vyakofya mbele ya Mwenyezimungu, kwa nfano, ewo wakiwoca wana wawo wakiwatenda  kafala ya maswanamu. Ntamana, Mwenyezimungu aakisaka kuwa wanu wake wawalande Wakanã, basi akiwatuma wanu wake kuwapoteza wanu wa Kanã.

**5. Kushanga ka wanadamu**
"Konta mawazo angu siyo sawa-sawa na mawazo enu, wala njila zenu sinjila zangu, kaamba Mola. Kamba bingu vyazili julu baidi pakulu kupunda aldhi, njila zangu novyo nlefu pakulu koliko njila zenu, mawazo angu makulu koliko mawazo enu umwe-po." (Izaya 55:8-9)

Mawazo a wanadamu matoto pakulu walimba kweleliwa na mawazo a Mola! Ndi ntamana, wanu wakatala ukweli wa Bibiliya konta awelewa.

**6. Ukipofu wa Lohõ**
Insa kamba: "Nukwambila kweli-kwelini kuwa munu saapongoliwe mala ya pili, asiyelele kuwa Mwenyezimungu akuwa nfalume wa mainsha ake." (Yáhaya 3:3)
"Sambi, munu saalongoziwa na Lohõ wa Mwenyezimungu aamini vinu vija na Lohõ wa Mwenyezimungu; kwake iye, vinu vya utolu. Iye eleliwa konta isakikana Lohõ wa Mwenyezimungu kunfafanulila." (1 Kolintiyu 2:14)
Wanu sawalungane na Lohõ wa Mwenyezimungu vipofu wa lohõ zawo, awakidili kweliliwa na ukweli.

## F. Kumaliza

Ofwe Wafúlati wa Insa tisakula tiwe wanu wa kweli. Atisakula kufisa vinu vyakuliga-liga kwelewa vilipo mBibiliya. Fala kusema ukweli,



## A. Mwanzo

Wesilamu wengi awakubali kuwa Bibiliya kitabu kimoja cili na ukweli wa Mwenyezimungu. Ingawa kwa hakika Kolowani ikwakikisha ukweli wa Maandiko Matakatifu a wenye kunfulata Insa Klistu, Maisilamu wakwamba kuwa Maandiko Matakatifu apinduliwa. Ewo wabuni javi konta maala mwingi mwawenye, Bibiliya ísema kinu ca kusiyana na vyandikiwe nKolowani. Vitabu viwili avilanda kuwa kesusa munu mmoja noyo ikiwa kulawilila kusiyana kitabu kimoja na cenziwe. Bibiliya isema (mu Isabu 23:19):

> "Mwenyezimungu siyo mwanadamu kuwa alongopa,
> wala siyo mwana wa mwanadamu kuwa atubiya.
> Vikúwa iye kwamba kinu saatendile?
> Au asowela kinu soolote kutenda noco?"

Sambi, tambe mwaja? Bibiliya ndi iséma ukweli au Kolowani ndi iséma ukweli. Kwa kusakula kongongola tafauti-yi, Wesilamu wengi wawasowelela Wafúlati wa Insa javi: "Bibiliya-yo ipinduliwa!" Fala usowezi wa javyo awongongola tafauti. Ofwe tisakula toolote kuwa kweli-kwelini vyawasowela-vyo sivyo vyakweli, Bibiliya ifãi kufyomiwa.

Ikiwa kweli, vitabu viwili-vi usemi wawo siwo mmoja, ikuwa konta kimoja acisuke ka Mwenyezimungu. Uwe újuzi ulamule julu ya kufyoma vitabu viwili-vi, usilamule kwa kunsowelela mwenziwo visaka kuwa vyoonse.

**Mifano ya kusiyana nkati ya Bibiliya na Kolowani**

1. Kolowani ísema (Súla 11:42-43) kuwa nabii Nnu ákiwanawo mwana mmoja, neyo mwanawe-yo kâzama na maji a mwanalukaya. Fala Bibiliya ísema (Mwanzo 6 na 7) kuwa nabii Nnu ákiwanawo wana watatu, anta mwana mmoja aapo azamile na mwanalukaya.

2. Kolowani ísema (Súla 6:74) kuwa wawaye Ibulahima ákitiwa Azali, fala Bibiliya ísema (Mwanzo 11:31) kuwa wawaye Ibulahima ákitiwa Tela.

3. Kolowani ísema (Súla 28:8-9) kuwa muka wa Filyauna ndi antulile Musa kuwa mwanawe. Fala Bibiliya ísema (Kulawa 2:5-10) kuwa mwana wa Filyauna muka ndi antwalile Musa akintenda kuwa mwananwe.

4. Kolowani ísema (Súla 28:38) kuwa Filyauna kamwambila Hamani kuwa ajenge ukuta nlefu ipate akwele oke ka Mwenyezimungu wa nabii Musa. Kusema kweli, ukwambiwa ukuta wa Babeli fala ewo ujengiwa baidi futi na Miswili, na ujengiwa myaka miya pansi-pa saanapongoliwa Filyauna. Na Hamani kainshi myaka miya kenda bandi ya kufwa Filyauna!

5. Kolowani ífunda kuwa Maliyamu mamaye Insa Wazili-Ilahi, ákiwa nlumbuwe Aluna (nduye Musa) na mwana wa Amulani. Bibiliya isema kuwa noyu Amulani-yu ndi âwele wawayawo Musa na Aluna. Musa ákiwa alu-ye Insa?
Zina la Máliyama lilandana na la Maliyamu, na kweli-kwelini Máliyama ákiwa nlumbuwe Aluna, fala kainshi kiyasi ca myaka 1400 Insa saanapongoliwa.

6. Kolowani (Súla 22:34-37) ísema kuwa kafala kinu cema kuntendela Mwenyezimungu, fala nyama na damu sivyo bola ka Mwenyezimungu, ila kinu bola ka Mwenyezimungu ndi utungu wawo wale wenye kutenda kafala. Fala Bibiliya ísema sana-sana maala mwingi mwawenye (kwa nfano, Lev. 16:17-20) kuwa damu ya kafala bola pakulu konta ndi namuna ya kulavya madambi etu. Na ísema novyo kuwa kafala yaalipeleke Insa Wazili-Ilahi, wakwitiwa ‘Kondoo wa Mwenyezimungu’,

> “Kwa kulipeleka mala moja noyo tu basi, káwalavya mizigo ya madambi awo milele wale wenye kwamini kuswamiiwa julu yake.” (Waeblaniya 10:14)

> “Iye kálawilila mala moja kwa milele. Iye kâja kutilavya mizigo ya dambi zetu, julu ya kulipeleka iye mwanyewe kuulaiwa akiwa kafala.” (Waeblaniya 9:26)



Kwa namuna mmoja noyo, walaka za Bibiliya zandikiwe na makono zikijuzi zinukuliwe konta mákina a kwandika awoneleliwa sekulu kumi na saba. Wakinukulu-wo, wakinukulu sana-sana kuno wakitunza. Walaka nyingi zakunukuliwa ziinshi mpaka lelo (kwa nfano, Nshokoto ya Baali ya Kufwa). Walaka za Bibiliya zanzile kwandikiwa na makono azipo.

Ingawa atina walaka zanzile kwandikiwa, tijuzi tamini kuwa vitabu vinukuliwe vyatili kutumila vyakweli konta vingi na piya vísema usemi mmoja nowo kimoja na cenziwe.

Vyengine vinukuliwe na makono vyanawo makosa matoto fala laisi kuwonelela. Makosa-yo awoneka kwa kutunza na vitabu vyengine. Tafauti nyingi zakulandana zilipo mBibiliya tiwona isabu basi. Kwa nfano, nfalume Joakim akiwanawo myaka nane ya ilimu wakati wanzile kutawala, kamba vyacamba kitabu ca pili Kolonika 36:9 fala usingana maala pengine cikwamba akiwa na ilimu ya myaka kumi na nane kitabu capili ca wafalume 24:8. Luga ya Kiyeblaniya yanziwe kwandikiwa kitabu ca Tauleti wakitumila kwandika isabu na alufu, na nozi alufu-zi vyazandikiwe-vyo zilandana na isabu za kulandana (kwa nfano, 8 na 18). Ndi ntamana, iwa laisi kulawilila makosa, fala kusema kweli, makosa-yo ákiwa aba.

**2. Kufasuli**
Kuwapo kufasuli jisi-jisi ka Bibiliya kamba vyaili Kolowani. Tauleti ili mBibiliya yandikiwa na luga ya Kiyeblaniya na Injili ili mBibiliya yandikiwa na luga ya Kigelegu. Ifasuliwa, na mpaka lelo yankufasuliwa kwa luga nyingi ipate wanu piya wejiwe ukweli wa Mwenyezimungu nkati ya luga zawo zawapongoleliwe wanyewe. Piya tafasuli za Bibiliya ziwa sana-sana fala ziwapo zisiyane kwa namuna za masowelelo.

**3. Kukwelela Bibiliya caputu**
Mala nyingi kuwapo kusiyana caifunda Bibiliya na mawazo a wanadamu, na noci ndi cilavizila umani.

malwazo, wa moyo wa kuhuzunika. Piya wakipata kupona na kupumuzika.

Kwake iye, inawa vinu vyake piya vyatendile wema vyandikiwa, duniya izima-i pasipatikane pakutula vitabu-vyo. Basi, Insa ákiwa mwananlume-wa kuwa javi, na Mwenyezimungu novyo javi ndi vyaali.

Ikisa Insa kafwila pansalaba, ipate alavye dambi mulumwengu-mu, kalawilila kuwa Nvushi wa wanadamu. Ikisa tena Insa kafufuka ka wafwi na kawa hai mpaka lelo. Siyo munu wa kutambuliwa muhadisi basi, kwasa javyo ndi munu hai.

Insa ndi munu bola pakulu nkati ya Hadisi ya ulumwengu, na nguvu maalumu piya ulumwengu wa lelo-wu. Piya usowezi wa Bibiliya untula Insa kati-kati pamoja na tamã yake ya uhai wa milele, ituliwe ka wale wenye kumwamini iye.

Bibiliya yandikiwa ipate wanadamu wankubali Insa na welewe kuhusu iye, ikisa wampende na wanfulate Insa Wazili-Ilahi.
Ofwe tíjuzi titondole kinu catiwona kuwa bola pakulu, kunkubali au kunkana Insa Wazili-Ilahi. Tikinkubali Insa, tikuka kuwa na mainsha a milele binguni; tikinkatala Insa, tikúka kutabika milele motoni.
Kinu bola pakulu kwa kila munu ndi kutondola mwanyewe kumpokelela au kunkatala Insa.

## E. Tafauti za mBibiliya

**1. Kunukulu**
Lelo viliga-liga kusingana buku linukuliwe kwa myaka miyateni ipitile. Likiwepo buku javyo, sunga sana-sana, novyo-sivyo alasa kuwa na kasolo nanga liwa na tafauti mmojiwapo kupapuka-papukanga au kutopela konta ya kwikala wingi wa suku. Isakikana kuludila kunukulu ipate lisipoteye na mwinsho kuja kulainika nfululu.



7. Kolowani (Súla 4:157) ísema kuwa Insa aaulaiwe wala agomezeliwe pansalaba; evi visiyana na vyaisema Bibiliya maala mwingi mwawenye. (Kwa nfano: Matwaya 27; Malku 15; Luka 23; Yáhaya 19).

8 Kolowani (Súla 5:116) ísema kuwa Utatu wa Mwenyezimungu uwa javi: Insa na Maliyamu mamaye Insa, pamoja na Ilai! Usemi-u siwo wakweli; Muhamadi eleliwe sana wakati wakifunda kuhusu Utatu wa Mwenyezimungu. Bibiliya ifunda kuwa Utatu wa Mwenyezimungu ndi javi: Mwenyezimungu Baba, na Mwenyezimungu Mwana, na Mwenyezimungu Lohõ Takatifu. Mwenyezimungu mmoja alolota kwa wanu watatu (Matwaya 3:16; 28:19).

**Kolowani ikweleza kinani kuhusu Bibiliya?**

1. Isilamu ájuzi akubali piya vyawasemile minabii wapitile (Súla 2:136; 4:136; 29:46). Fala sambi catiwona ndi kuwa Maisilamu wengi awakubali, wakwamba avina faida na vipinduliwa.

2. Nozo habali za mida-zo ndi zaapewe nabii Ibulahima na nabii Isaki na nabii Yankubu na nabii Musa pamoja na Bwana Insa.
(Súla 2:136)

3. Kolowani ísema (Súla 2:136): “Tisitule namuna ya kusiyana moja na nyenziwe”. Basi sambi, Kolowani aitondola ezo habali zolotiwe-zo.

4. Kolowani ikwakikisha habali zoolotiwe mida (Súla 3:3; 5:49; 10:37; 4:47) fala novyo-sivyo, ikaidi vinu vya usemi maalumu.

5. Vitabu vya mida sainesuka Kolowani, Muhamadi vînfãi kutumila. (Súla 10:94; 3:93; 21:7; 3:71) Muhamadi kâwa munu mmoja wa kusunga vitabu vya mida. (Súla 5:48) Kolowani anta pamoja aisema kuwa Bibiliya ipinduliwa.

**Tisaka tukudailini kwa inshima wanduzetu Maisilamu**

### 1. Wakatini waidanganyiwe au waipinduliwe Bibiliya?

Iwapo nafasi ya kujibu majibu mawili basi kuhusu kudaili-ku:

a) Bibiliya ipinduliwa saanapongoliwa Muhamadi. Kinu-co acikidilika, kamba vyaisema Kolowani yawenye.

b) Bibiliya ipinduliwa Muhamadi paafwile. Neci novyo acikidilika konta piya walaka zitumiliwe kwa kutungiwa tafasili ya Bibiliya, zíkiwepo myaka miya pansi -pa kabula ya Muhamadi.

### 2. Nani apindule Bibiliya?

Iwapo nafasi ya kujibu majibu mawili tu basi kuhusu eku kudaili-ku:

a) Bibiliya ipinduliwa na wanadamu wema au malaika. Eci acikidilika konta wanadamu wema na malaika wamopa Mwenyezimungu na awakisaka wala awakijuzi kunkeshefu Mwenyezimungu.
Nowo wanu-wo pamoja na malaika wakwamini habali ya nguvu ili mwinsho wa Bibiliya, Mwenyezimungu pambile javi:

> "Omi nisema kweli ka wanu piya wasikila kubushulu ka eci kitabu-ci: Ikiwa munu kengeza kinu kimoja, Mwenyezimungu amwengeza hukumu yake yandikiwe nkati ya noci kitabu-ci. Na ikiwa munu kalavya usémi usaka kuwa wonse ubushuliwe nkati ya eci kitabu-ci, Mwenyezimungu anlavya upande wake wa Muti wa Uhai, na wa sidadi takatifu, vyandikiwe nkati ya noci kitabu-ci." (Apoc.22:18,19)

b) Bibiliya ipinduliwa na wanadamu wabaya au mashetwani. Kinu-ci acikidilika novyo konta wanadamu wabaya na mashetwani awasaka wala awakidili kutunga kitabu kamba Bibiliya. Kweli-kwelini, Bibiliya ikweleza kuwa munu ájuzi ampende Mwenyezimungu na jilani wake; novyo, Bibiliya ikataza dambi piya, na iwalaumu wanu wabaya wonse pamoja na mashetwani, iwengiza motoni kwa daima milele. Ndi ntamana mashetwani awasaka kutunga kitabu kamba Bibiliya.

### Juwabu limoja basi?

Mwenyezimungu Mwenye uwezo piya pamoja na wijiwifu singali kasaka kupinduliwa usemi wake!



ukweli, na ndi nowo ulikunusulu wanu wengi wawenye watendiwe utwana. Ewo wakiwa watwana kwa sababu ya dambi na shetwani na kwa koopa kifo na kwa koopa majini na kadalika. Wawapo iliki ya wanu wakidili kwakikisha kuwa usemi wa Mwenyezimungu uwapindulanga wanu na kuwombola.

**Kumaliza?**

Piya-vi vikwakikisha sana-sana ukweli wa Bibiliya. Ofwe tiwanawo shaliya pakulu kutumaini piya vyaisema Bibiliya. Aye, mpaka na tamã zawo za maajuza kuhusu mainsha atili nawo-ya na mpaka a mbele.

## D. Bibiliya ikwamba kinani?

Insa ndi sina la Bibiliya kamba moyo vyauwa sina la mwili. Tauleti (ndi upande wa Bibiliya yoolotiwe Insa saanapongoliwa) ikweleza taifa, taifa ya Izilaeli. Injili (itungiwe bandi ya Insa) ikweleza kuhusu mwananlume mmoja. Mwenyezimungu katula noyo taifa-yo ipate ampe noyo mwananlume-yo mulumwengu-mu.
Mwenyezimungu mwanyewe kalawilila kuwa mwanadamu Insa, ipate wanadamu weleliwe sana-sana vyaali Mwenyezimungu. Insa sawa-sawa na Mwenyezimungu. Insa ákiwa Nlungu kâlipindula akiwa mwanadamu ipate awafãi wanadamu. Kulawilila ka Insa duniya-i ndi kinu bola pakulu nkati ya piya Hadisi. Tauleti itengeza kuja ka Insa; Injili ikweleza kuhusu Insa.

Kamba mwanadamu, Insa kainshi mainsha maalumu mema akwijiwikana. Iye akiwa mwananlume mwema sana na múminu pakulu, na wa imani pakulu na wa huluma pakulu.

Insa akiwapenda wanu. Vikinkima kuwawona wanu wakimíwe, kukimwajibu kuswamii. Kukimwajibu kusaidiya; akitendanga maajuza a matajabisa apate kuwapa cakulya wenye kuwakola njala. Kuwanusulu wenye kutabika mpaka akiliwala kulya. Wanu wengi wakija kwake iye-junudi ya wanu wakusokela, wakushindiwa na

vitolotela namuna vyawakiinshi wanu wa mida. Ewo wankuwonelela vinu vyakwakikisha ukweli wa Bibiliya.

Vinu bola pakulu viwoneleliwe ndi vile vitiwa “Nshokoto wa Baali ya Kufwa”. Viwoneleliwa mwaka 1947 na wanemba wamoja walabu wakipita wakinsakula mbuzi wawo asike. Ewo wengila njonga, wakisingana mivulo ya utope, nomo ikiwepo mishokoto na usemi wakwandikiwa javi. Wataalamu pamoja na wanlimu wa Hadisi na wa luga walifyomesa na wangali wakilifyomesa na kufasuli noci mwana kinu-ci. Noyo mishokoto-yo yanawo walaka za piya mabuku a Tauleti mBibilya ila kitabu ca Eshteli ndi sacipo. Vyandikiwa mmasambala (msambala a ng'ombe) na papylus (namuna ya walaka zakutendiwa za muti) na mpaka na za shaba. Nshokoto mmojiwapo wandikiwa kitabu ca kutimu cawenye ca nabii Izaya myaka miyateni Insa Wazili-Ilahi sanesuka; ciwa sawa-sawa na piya vinu vilipo mBibiliya ilipo mpaka sambi-pa-yi.

#### Ushahidi wa binafsi wa wenye kutunga Hadisi za mida

Mwenye kutunga Hadisi wakusifiwa pakulu koliko piya-wo âkiwa Koloneliyu Tasitus. Iye kwawo Loma, aakintumika Mwenyezimungu. Sekulu ya kwanza yawenye, iye katunga usemi wa kwamba javi: “Nkati ya ufalume wa Tibeliyu, Pontiyu Pilatu amulaya Klistu ...”

Kwa javyo, eyo mwenye kutunga Hadisi-yo, munu saana dini, kakikisha kifo ca Insa Wazili-Ilahi. (Zina lengine la Wazili-Ilahi ndi Klistu.).

Na novyo sekulu ya kwanza-yo, Yahudi mmoja wakwitiwa Sefu, mwenye kutunga hadisi za mida, mbuku mwake (“Úmida wa Mayahudi”) uwapo ushahidi wa kwakikisha kugomezeliwa na kufufuka ka Insa.

#### Ukweli wa Bibiliya ukólotiwa nkati ya mainsha a wenye kwamini

Safali moja Insa kaamba: “Basi mukuja kwijiwa ukweli, na ukweli nowo ukunusuluni.” Usemi wa Mwenyezimungu ulipo mBibiliya ndi



## B. Bibiliya yolotiwa kinamunani?

Namuna ya kufafanuliwa Bibiliya isiyana pakulu futi na kufafanuliwa ka Kolowani. Kamba vyaisakikana dini ya Kiisilamu, Kolowani ndi “nazil”, maana ake ‘isuka kwa luhuya’. Wesilamu wakwamba kuwa Kolowani isungiwa nluwawo binguni, na ikitelemusiwa kipande-kipande na laika wakwitiwa Jibulilu muda wa myaka shilini na kinu. Kwasa javyo, Bibiliya yandikiwa na wanu alubaini jisi-jisi, piya-wo kila mmoja akifahamishiwa kila kinu na Lohõ wa Mwenyezimungu (2 Timotiyu 3:16), kwa muda kiyasi ca myaka elufu moja na miya sita (1600). Kwasa kulawa binguni, kwa usemi ujile na wanadamu; Bibiliya ísema javi:

> “Kinu bola pakulu ndi kukumbukila kuwa anta kubushulu kumojiwapo ka Maandiko Matakatifu siyo tafasili ya mawazo a munu mwanyewe tu basi. Konta vibushuliwe-vyo avyeleziwe kwa nafsi ya wanadamu, falakini wanadamu watakatifu wa upande wa Mwenyezimungu wasowela kwa kupewa fahamu na Lohõ Takatifu.” (2 Pedulu 1:20-21)

Nang'anizani sana-sana; usemi-u ukwamba: “Wanadamu watakatifu wa upande wa Mwenyezimungu wasowela.” Kusema kweli, ‘kusowela’ ndi kinu ca wanadamu. Ntamana Mwenyezimungu kawatumila wanadamu akiwapa usemi wake. Na novyo, eya Maandiko-ya akwamba kuwa ewo “wafahamishiwa kila kinu na Lohõ Takatifu.” Neco ndi kinu ca kulawa binguni. Basi, kwa evi vitabu-vi, tiwanawo kitabu kimoja ca kusiyana. Usemi uli mBibiliya ndi:

- usemi wa binguni
- ukifafanuliwa aba-aba
- weleziwa julu ya wanadamu
- wanawo namuna nyingi zawenye za Maandikilo fala piya-yo ásema habali moja noyo.
- masemo ake andikiwa na wanu alubaini jisi-jisi fala alanda kamba andikiwe na munu mmoja basi; kusema kweli, andike mmoja basi – kandika Mwenyezimungu.

Ndi ntamana, tangu mwanzo mpaka mwinsho wa ukulu wake, akupo kusiyana. Kupewa fahamu na Lohõ Takatifu maana ake siyo kuwa Mwenyezimungu usemi wake akiwafyomela wandishi, wanadamu kubaki sawana mawazo. Sivyaviwele javyo, Lohõ Takatifu ndi akiwesusila wanu ankili ya kuwakumbusa, kusema kila kinu. Kwa namuna-i akilavya habali kamili ya luhuya, na kwa mpunde mmoja nowo, akinlongoza mwandishi namuna ya kwandika.

Sodali ya kuwepo kusikizana ka luhuya na wanadamu kwa kutunga habali mmoja ya binguni ikwijiwiwa sana-sana ingawa viliga-liga kweleza. Kamana kulungana ka lohõ na mwili wa munu ndi sili ulu pakulu, anta paiwa munu-yo mwijiwifu pakulu, vilimba futi kweleliwa; kweleliwa kulungana na Lohõ wa Mwenyezimungu pamoja na lohõ za wanadamu!

Ingawa atijiwa vyayenenda luhuya, tiwankuwona ushahidi wake julu ya kubushulu ka Bibiliya. Kubushulu kukweleza vinu vya mbele, na tiwankuwona kutimiziwa kwawo; kubushulu kutimiziwe ndi ushahidi nkulu kuwa wanadamu wápewa fahamu ya kila kinu na Lohõ Takatifu.

## C. Ushahidi

#### Kubushulu kutimíziwe

Nkati ya Bibiliya kuwapo kubushulu kwingi kawenye kutimiziwe kweli-kwelini. Tikweleza kubushulu kwengine-po kulipo emu:

1. Kubushulu kubushuliwe maala paakija kupongoleliwa Insa kweleziwa myaka miya saba saanapongoliwa Insa (Mikeya 5:2) na kutimiziwa nfululu. (Luka 2:1-7)

2. Kubushulu kubushuliwe kupongoliwa ka Insa na mwali wa bikila kweleziwa myaka miya saba saanapongoliwa Insa (nabii Izaya 7:14) na kutimiziwa nfululu. (Matwaya 1:18-23)



3. Kubushulu kubushuliwe kuwa Insa akija kuvusha na kuponesa, eko kweleziwa myaka miya saba saanapongoliwa Insa (Izaya 35:4-5) na kutimiziwa nfululu. (Matwaya 1:21; Luka 19:10; Yáhaya 3:13-21)

4. Kubushulu kubushuliwe Insa kwingila Yelusalemu akilinyenyekeya ampandile kabulu kweleziwa myaka miya nne na amusini Insa saanapongoliwa (Zakaliya 9:9) na kutimiziwa nfululu.
(Matwaya 21:1-9)

5. Kubushulu kubushuliwe kuyeleliwa Insa kweleziwa myaka 480 Insa saanapongoliwa (Zabuli 41; Zakaliya 11:12-13) na kutimiziwa nfululu. (Malku 14; Matwaya 27:3-8)

6. Kubushulu kubushuliwe kuhusu tabu za Insa pamoja na kifo cake cakugomezeliwa pansalaba kweleziwa myaka miya saba Insa saanapongoliwa (Izaya 53; Zabuli 22:1-18) na kutimiziwa nfululu. (Yáhaya 19)

7. Kubushulu kubushuliwe kufufuka Insa ka wafwi kweleziwa myaka miya Insa saanapongoliwa (Zabuli 16:8-10) na kutimiziwa nfululu. (Luka 24:11)

Aalawilila wa kukidili kukaidi ushahidi wa evi piya vibushuliwe na vitimiziwe-vi; Bibiliya ndi kitabu kimoja nkati ya piya vitabu vya dini cilinawo vyakubushuliwa. Na vibushuliwe-vyo piya visa kutimiziwa nfululu.
Kwasa ushahidi nkati ya Bibiliya (vibushuliwe vikisa kutimiziwa), uwapo ushahidi mwengine wakuwoneka; ushahidi-wu ndi watisaka kuwona sambi-wu.

#### Kuwoneleliwa ka vinu vya mida

Sini pansi ya aldhi maala mwingi mwawenye kati ya Izilaeli na inti jilani viwapo viluwi vingi vyawenye vya koolota kusilimuka ka mida. Viluwi-vyo visimbiwanga, na wataalamu wengi wawenye wankutendela ufyomi, wanu wakunfulata Insa na wengine sawanfulata Insa. Wataalamu-wo wawonelela vinu vingi vyawenye pansi ya aldhi